NSW GOVERNMENT Health
South Eastern Sydney
Local Health Network



# KICHOCHO

SCHISTOSOMIASIS

## Kichocho ni nini? (What is Schistosomiasis?)

Kichocho, hujulikana pia kama kisonono cha damu, ni ugonjwa unaosababishwa na minyoo midogo sana inayoishi kwenye maji baridi

- Ambukizo hutokea wakati ngozi yako inapokutana na minyoo mitoto
- Minyoo inaweza kuingia kwenye ngozi na kusafiria kwa mapafu na ini, panapokua minyoo mizima na kuanza kuzaa mayai
- Minyoo inaweza kuishi mabomba ya damu, kibofu cha mkojo, au matumbo kwa miaka mingi
- Isipotibiwa, minyoo na mayai yao inaweza kuathiri ini, matumbo, na kibofu. Mara chache, inaweza kusababisha matatizo kama kifafa (shtuko la moyo).

## Nani ana hatari kuambukizwa? (Who is at risk?)

- Kama umeishi, au umesafiri kwenda mahali panapoishi minyoo ya kichocho katika maji baridi (k.m., katika nchi zingine za Afrika, Bamba la Karibi, China kusini, Asia kusini-mashariki na Mashariki ya Kati), unaweza umeshaambukizwa zamani
- Watu wanaambukizwa wakati wa kufanya shughuli kama kuchota maji, kulima au kuvua samaki katika miferji, mito na maziwa ya maji baridi.

## Dalili ni nini? (What are the symptoms?)

- Baada ya masiku kuambukizwa watu wengine hugundua vipele au ngozi inayowasha
- Wakati wa wiki chache ijayo, inaweza kutokea homa, kichwa kuumwa, kohozi na maumivu ya misuli
- Watu wengine hawatakuwa na dalili, zozote hata kama minyoo inaishi ndani mwili wao na kuzaa mayai.

## Inatambuliwa jinsi gani? (How is Strongyloides detected?)

- Kipimo cha damu kitaonyesha kama umeshawahi kuwa na kichocho wakati wowote
- Kama jibu la kipimo linaonyesha minyoo, unaweza kuombewa kutoa sampuli ya mkojo na choo kuangalia kama kuna mayai yoyote
- Kama mayai yakionekana, vipimo vingine (km eksrei) vinaweza vitahitajika.

## Maambukizo yanaweza kutibiwa jinsi gani? (How is the infection treated?)

- Madawa ya salama na ya kufaa yanapatikana kwa kutiba kichocho
- Watu wengi wakipata kipimo cha damu kinachoonyesha minyoo watapewa vidonge
- Kama mayai yakionekana katika mkojo au choo chako, kozi ya pili ya matibabu inaweza kuhitajika

Maelezo zaidi yanapatikana kwan (Further information is available from)

April 2011